**Hati ya Taarifa Muhimu**
***Kusudi:*** *Hati hii inakupatia taarifa muhimu kuhusu bidhaa hii ya uwekezaji. Hii si hati ya kibiashara.*
*Taarifa hii imetolewa kwako kwa mujibu wa wajibu wa kisheria ili kukusaidia kuelewa asili ya bidhaa hii pamoja na hatari, ada, faida na hasara zinazoweza kuhusishwa nayo na kukusaidia kuilinganisha na bidhaa nyingine.*

## Bidhaa

# FCPE L'OREAL – MPANGO WA HISA KWA WAAJIRIWA 2026

*Kampuni ya usimamizi: Amundi Asset Management (tangu sasa ni "sisi" au "Kampuni ya Usimamizi"), sehemu ya kikundi cha kampuni za Amundi.*
*990000210419 – Sarafu: EUR*
*Tovuti ya Kampuni ya Usimamizi: www.amundi.fr*
*Piga simu +33 143233030 kupata maelezo zaidi.*
*Mamlaka ya masoko ya fedha ya Ufaransa (Autorité des marchés financiers – AMF) ina jukumu la kusimamia Amundi Asset Management kuhusiana na Hati hii ya Taarifa Muhimu.*
*Amundi Asset Management imesajiliwa nchini Ufaransa chini ya n°GP-04000036 na inadhibitiwa na AMF.*
*Tarehe ya kuanzishwa kwa Hati Hii ya Taarifa Muhimu: 09/01/2026*
***Unakaribia kununua bidhaa ambayo si rahisi na inaweza kuwa vigumu kuelewa.***

## Je, hii ni bidhaa gani?

**Aina:** Bidhaa hii ni mfuko mbadala wa uwekezaji (FIA) ulioanzishwa kama hazina ya pamoja ya kumiliki hisa ya wafanyakazi (FCPE), inayosimamiwa na sheria za Ufaransa.

**Kipindi:** FCPE hii imeundwa kwa muda usio dhahiri. Kwa idhini ya Bodi ya Usimamizi ya FCPE, Kampuni ya Usimamizi inaweza kuunganisha, kugawanya au kufilisi FCPE. FCPE pia inaweza kufutwa katika hali ambayo vitengo vyote vimekombolewa.

**Malengo:** FCPE ni hazina ya muda ("FCPE relais"). Iliundwa ili kujisajili kwa ongezeko la mtaji lililohifadhiwa kwa wafanyakazi wa L'OREAL.

Kabla ya uwekezaji kwenye hisa za kampuni, kiasi kilichopokelewa kitawekezwa kulingana na mbinu ya busara. Usimamizi huu unahusisha hatari ya kupoteza mtaji, hatari ya kiwango cha ubadilishaji na hatari ya mkopo.
Kufuatia kujisajili kwenye ongezeko la mtaji kupitia FCPE, lengo litakuwa ni kufuatilia kupanda na kushuka kwa hisa za L'OREAL, ambapo uwekezaji utafanyika. Kwa hivyo, FCPE inaweza kuwa chini ya hatari ya hasara ya mtaji na hatari mahususi ya hisa zisizo na riba ya kudumu inayohusishwa na mkusanyiko wa uwekezaji katika dhamana za kampuni moja. **FCPE inakusudiwa kuunganishwa, hivi karibuni, kuwa "MPANGO WA HISA WA WAFANYAKAZI" FCPE, hazina ya pamoja ya kumiliki hisa ya wafanyakazi iliyoainishwa katika kategoria ya "FPCE iliyowekezwa katika dhamana zilizoorodheshwa za kampuni" (Hati ya Taarifa Muhimu ya FCPE hii imeambatanishwa na hati ya sasa).**

Viashiria vya hatari na hali za utendaji zilizotajwa katika Hati hii ya Taarifa Muhimu zinatokana na data kutoka kwenye hazina ya pamoja ya kumiliki hisa ya wafanyakazi FCPE ya "L'OREAL - MPANGO WA HISA KWA WAAJIRIWA 2026" FCPE inakusudiwa kuunganishwa.

**Kalenda ya kutoa:**
Bei ya kujisajili: Bei itakuwa sawa na wastani wa bei za ufunguzi wa hisa za L'OREAL wakati wa Euronext Paris katika kipindi kinachoanzia tarehe 8 Mei, 2026 hadi 4 Juni, 2026, ikijumuisha, punguzo la chini la 20%.
Tarehe ya kutangazwa kwa bei ya kujisajili: 5 Juni, 2026
Kipindi cha usajili: kuanzia tarehe 10 Juni, 2026 hadi 24 Juni, 2026, kwa pamoja.
Tarehe ya kuongeza mtaji: Terehe 30 Julai, 2026.
Tafadhali rejea kanuni za FCPE kwa hali ambapo usajili utapunguzwa ikiwa utazidi kiasi kilichotengwa kwa ajili ya kuongeza mtaji.
Mapato na faida halisi ya mtaji lazima ziwekezwe upya.
Unaweza kuomba fidia ya vipande vyako kila siku, maombi ya fidia hutekelezwa kila siku kwa mujibu wa hali zilizowekwa katika kanuni za FCPE.

**Mwekezaji wa rejareja:** Bidhaa hii imelenga wawekezaji ambao ni wanufaika wa mpango wa akiba kwa wafanyakazi, ambao wana ukomo au hawana maarifa ya msingi na/au uzoefu wa kuwekeza kwenye mifuko, ambao wanalenga kuongeza thamani ya uwekezaji wao kwa kipindi cha uwekezaji kilichopendekezwa, na ambao wako tayari kukabiliana na kiwango kikubwa cha hatari kwenye mtaji wao wa mwanzo.
Bidhaa hii haiko wazi kwa wakazi wa nchini Marekani / *Watu wa US* ("ufafanuzi wa "Watu wa US" unapatikana katika tovuti ya Kampuni ya Usimamizi kwenye www.amundi.com).

**Maelezo ya ziada:** Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu FCPE pamoja na kanuni na ripoti za kifedha, kwa lugha ya Kifaransa, bila malipo, kwa kutuma maombi kwa: Amundi Asset Management - 91-93 boulevard Pasteur, 75015 Paris, France.
Thamani kamili ya mali za FCPE inapatikana kwenye www.amundi-ee.com.

**Mhifadhi amana:** CACEIS Bank.



C1 - Matumizi ya ndani

## Je, hatari ni zipi na ninaweza kupata nini kama malipo?

**KIASHIRIA CHA HATARI**

| 1 | 2 | 3 | 4 | **5** | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|

Hatari ya chini kabisa ← → Hatari ya juu kabisa

Kiashiria cha hatari kinasadiki kwamba unashikilia bidhaa kwa miaka mitano.

Inaweza kukuwia vigumu kuuza bidhaa au unaweza kuiuza kwa bei ambayo itaathiri kiasi cha malipo utakayopokea.

Mjumuisho wa kiashiria cha hatari hutumika kutathmini kiwango cha hatari ya bidhaa hii ukilinganisha na bidhaa nyingine. Huonyesha uwezekano wa bidhaa hii kupata hasara katika hali ya kubadilika kwa masoko au uwezekano wa kushindwa kukulipa.

Tumeainisha bidhaa hii kuwa 5 kati ya 7, ambayo ni ya hatari ya daraja la kati hadi la hatari kubwa. Kwa maneno mengine, hasara zinazoweza kutokea kuhusiana na utendaji wa bidhaa za siku zijazo ni za kati hadi za juu, na ikiwa hali ya soko ingedorora, kuna uwezekano mkubwa kwamba uwezo wetu wa kukulipa utaathirika.
Zaidi ya hatari hizo zilizojumuishwa kwenye kiashiria cha hatari, hatari nyingine zinaweza kuathiri utendaji wa Hazina. Tafadhali rejea kanuni za FCPE za L'OREAL – MPANGO WA HISA KWA WAAJIRIWA 2026.
Hatari nyingine kuu hazijajumuishwa katika kiashiria:
Hatari ya ukwasi wa soko inaweza kuzidisha mabadiliko katika utendakazi wa bidhaa.
Hatari ya kuwekeza sehemu moja: ikiwa uwekezaji utafanyika katika mfuko mmoja na mfuko huo usifanye vizuri, hasara zinazopatikana zinaweza kuwa kubwa kuliko ambavyo zingekuwa iwapo kungekuwepo sera ya kuwekeza katika mifuko mbalimbali na/au katika masoko mengi zaidi.
Kwa kuwa bidhaa hii haijumuishi ulinzi wowote dhidi ya kutokuwa na uhakika wa soko la siku zijazo, unaweza kupoteza sehemu au uwekezaji wako wote.

## Hali za utendaji

Hali isiyofaa, ya kati na inayofaa zilizowasilishwa ni vielelezo vinavyotumia utendakazi mbaya zaidi, wastani na bora zaidi wa Hazina katika kipindi cha miaka 10 iliyopita. Masoko yanaweza kubadilika na kuwa ya tofauti sana katika siku zijazo. Hali ya mkazo inaonyesha kile unachoweza kufikia katika hali mbaya ya soko.

**Kile utakachokipata kutoka katika bidhaa hii kinategemea na utendaji wa soko siku zijazo. Mwelekeo wa soko siku zijazo si wa uhakika na hauwezi kutabiriwa.**

| Kipindi cha kukaa na bidhaa kilichopendekezwa: miaka 5<br>Uwekezaji wa € 10,000 | | | |
|---|---|---|---|
| **Hali** | | **Ikiwa utajiondoa baada ya mwaka 1** | **Ikiwa utajiondoa baada ya miaka 5** |
| **Kiwango cha chini** | Hakuna hakikisho na malipo ya kiwango cha chini. Unaweza kupoteza sehemu au uwekezaji wako wote | | |
| **Hali ya mkazo** | **Unachoweza kupata baada ya kukata ada** | € 1,960 | € 1,970 |
| | Wastani wa mapato ya mwaka | -80.4% | -27.7% |
| **Hali isiyofaa** | **Unachoweza kupata baada ya kukata ada** | € 7,550 | € 7,440 |
| | Wastani wa mapato ya mwaka | -24.5% | -5.7% |
| **Hali ya kati** | **Unachoweza kupata baada ya kukata ada** | € 11,320 | € 24,190 |
| | Wastani wa mapato ya mwaka | 13.2% | 19.3% |
| **Hali inayofaa** | **Unachoweza kupata baada ya kukata ada** | € 16,810 | € 33,080 |
| | Wastani wa mapato ya mwaka | 68.1% | 27.0% |

Tarakimu zilizoonyesha nzinajumuisha ada zote zinazohusiana na bidhaa.

Hali isiyofaa: Aina hii ya hali ilitokea kwa uwekezaji kati ya 29/12/2023 na 10/01/2025.
Hali ya kati: Aina hii ya hali ilitokea kwa uwekezaji kati ya 30/06/2017 na 30/06/2022.
Hali inayofaa: Aina hii ya hali ilitokea kwa uwekezaji kati ya 30/11/2016 na 30/11/2021.

## Je, nini kitatokea ikiwa Amundi Asset Management itashindwa kufanya malipo?

Bidhaa ni umiliki wa pamoja wa vyombo vya kifedha na amana unaojitegemea dhidi ya Kampuni ya Usimamizi. Katika hali ya kutofaulu kwa Kampuni ya Usimamizi, mali ya bidhaa inayoshikiliwa na amana haitaathiriwa. Katika hali ya kutofauli kwa mhifadhi amana, hatari ya upotezaji wa kifedha kutokana na bidhaa hupunguzwa kwa mgawanyo wa kisheria wa mali za mhifadhi amana mbali na zile za bidhaa.

## Je, ni ada gani zinazohusiana na uwekezaji?

Mtu anayeuza au kukushauri kuhusu bidhaa hii anaweza kukuomba ulipe ada ya ziada. Katika hali hii, mtu huyu atakueleza kuhusu ada hizi na jinsi zinavyoathiri uwekezaji wako.

### Ada kwa kipindi chote

Majedwali yanaonyesha kiasi ambacho hupunguzwa kutoka kwenye uwekezaji wako ili kufidia ada za aina mbalimbali. Kiasi hiki hutegemea kiasi cha uwekezaji uliofanya na kiasi cha muda utakaoshikilia bidhaa hii. Kiasi kilichoonyeshwa hapa ni mifano inayotegemea mfano wa kiasi cha uwekezaji na vipindi tofauti vya uwekezaji vinavyowezekana.
Sisi tumefikiria kwamba:
– katika mwaka wa kwanza, utarudisha kiasi ulichowekeza (0% za mapato ya kila mwaka). Kwa vipindi vingine vya kushikilia bidhaa, tumefikiria kwamba utendaji wa bidhaa ni kama ilivyoonyeshwa katika hali ya kati;
– € 10,000 imewekezwa.

| Uwekezaji wa € 10,000 | | |
|---|---|---|
| **Hali** | **Ikiwa utajiondoa baada ya miezi 3*** | **Ikiwa utajiondoa baada ya miaka 5**** |
| **Jumla ya gharama** | € 2 | € 40 |
| **Athari za gharama za kila mwaka***** | 0.1% | 0.04% |

*Muda uliokadiriwa wa hazina ya muda.


C1 - Matumizi ya ndani

** Kipindi cha kukaa na bidhaa kilichopendekezwa.
***Hii inaonyesha jinsi ada zinavyopunguza mapato yako ya kila mwaka kwa kipindi chote cha kushikilia bidhaa. Kwa mfano, inaonyesha kwamba ikiwa utajiondoa mwishoni mwa kipindi cha kukaa na bidhaa kilichopendekezwa, wastani wa mapato yako kwa mwaka unatabiriwa kuwa 19.40%, kabla ya ada na 19.32% baada ya ada.

## Muundo wa ada

| | Ada ya mara moja ya kuingia au kutoka | Ukijiondoa baada ya mwaka 1 |
|---|---|---|
| **Gharama za kujiunga** | Hatutozi gharama zozote za kujiunga kwa bidhaa hii. | Hakuna |
| **Gharama za kujiondoa** | Hatutozi gharama zozote za kujiondoa kwa bidhaa hii. | Hakuna |
| | **Ada zinazoendelea ambazo zinatozwa kila mwaka** | |
| **Ada ya usimamizi na ada nyingine za uongozi na uendeshaji** | 0.07% ya thamani ya uwekezaji wako. Huu ni ukadiriaji. | € 7 |
| **Ada za miamala** | Sisi hatulipishi ada za miamala kwa bidhaa hii. | Hakuna |
| | **Ada za ziada zinazotozwa chini ya masharti maalum** | |
| **Ada ya utendaji** | Sisi hatulipishi ada za utendaji kwa bidhaa hii. | Hakuna |

## Je, ninaweza kuishikilia bidhaa hii kwa muda gani na je, ninaweza kutoa pesa mapema?

**Kipindi cha kukaa na bidhaa kilichopendekezwa:** miaka 5. Kipindi cha kuishikilia kilichopendekezwa kinatokana na tathmini yetu ya sifa za hatari na zawadi na ada za FCPE. Kipindi hiki hakizingatii kipindi cha ufungaji kinachohusiana na mpango wa akiba kwa wafanyakazi.

**Ratiba ya maombi:** Wawekezaji wanaweza kuomba fidia ya vipande vyao kwa mujibu wa vigezo na masharti vilivyobainishwa kwenye kanuni za FCPE. Kwa kujiondoa kabla ya kipindi cha kukaa na bidhaa kilichopendekezwa kunaweza kuathiri utendaji uliotegemewa. Kampuni ya usimamizi inaweza kutekeleza utaratibu wa kuweka kikomo cha utoaji wa fedha kwa kipindi fulani (unaojulikana kama “Gates”). Vigezo na masharti ya ufanyaji kazi yamebainishwa kwenye Kanuni.

## Je, ninaweza kutoa malalamiko vip?

## Je, ninaweza kutoa malalamiko vipi?

Ikiwa una malalamiko yoyote, unaweza:
- kutuma barua kwa Amundi Asset Management au 91-93 boulevard Pasteur, 75015 Paris - France
- kutuma barua pepe kwa dic-fcpe@amundi.com

Tafadhali onyesha kwa uwazi taarifa za mawasiliano yako (jina, anwani, nambari ya simu au barua pepe) na toa muhtasari wa maelezo kuhusu malalamiko yako. Maelezo zaidi yanapatikana kwenye tovuti yetu www.amundi.fr na/au kwenye tovuti ya mmiliki wa akaunti yako.

## Maelezo mengine yanayohusika

Utapa kanuni, hati za taarifa muhimu, maelezo ya mmiliki wa vipande, ripoti za kifedha na hati za maelezo ya ziada kuhusu Hazina, ikijumuisha machapisho mbalimbali ya sera za Hazina, ikiwa ni pamoja na sera mbalimbali za Hazina zilizochapishwa kwenye tovuti yetu www.amundi.fr na/au kwenye tovuti ya mmiliki wa akaunti yako. Pia unaweza kuomba nakala ya hati hizi kutoka makao makuu ya Kampuni ya Usimamizi.
**Mmiliki wa akaunti:** Amundi ESR
Kutegemea na hali yako ya kodi, faida yoyote ya mtaji au mapato kutokana na kumiliki vipande vya FCPE inaweza kutozwa kodi.
FCPE iliundwa kama sehemu ya Kampuni na/au mpango wa akiba wa Kikundi, ambacho inahusika nacho na ambacho haiwezi kutenganishwa nacho. Imehifadhiwa kwa wafanyakazi na wanufaika wa toleo la hisa la mtoaji.
**Muundo wa Bodi ya Usimamizi**: Bodi ya Usimamizi imeundwa na hadi wawakilishi 4 wa washikilia vipande na wawakilishi 3 wa kampuni, ambao huteuliwa kwa mujibu wa kanuni za FCPE. Kwa maelezo zaidi, tafadhali rejelea kanuni za FCPE.
**Hali za utendaji:** Unaweza kurejelea hali za utendaji uliopita, zinazosasishwa kila mwezi, kwenye tovuti ya mwenye akaunti yako.
**Utendaji uliopita:** Unaweza kupakua utendaji uliopita wa Hazina kwa kipindi cha zaidi ya miaka 5 kutoka kwenye tovuti ya mwenye akaunti yako.



C1 - Matumizi ya ndani